### Mafunzo ya kitaalam

TTSA inaendesha kozi fupi zinazohusu utunzaji wa miti. Kama utunzaji wa bustani za miche ya miti Nursery techniques Course), jinsi ya kutambua miti (Field Identification Course) na ukweaji salama kwenye miti (Safe Tree Climbing Course). Wakala unatoa ushauri wa kitaalamu kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu Nyanja za mbegu za miti. Pia, TTSA ni kituo kikubwa cha mafunzo yanayohusu utaalamu wa mbegu za miti . Ni sehemu pekee katika Afrika Mashariki, Kati, na Kusini katika utoaji wa mafunzo ya ukweaji wa miti. Kutokana na shughuli zake, TTSA imekuwa kituo bora zaidi cha mbegu za miti katika kanda ya Afrika mashariki na kati. Ushauri wa kitaalam (Consultancy) TTSA inatoa ushauri wa kitaalamu na kufanikisha ukarabati wa mazingira yaliyoharibiwa kutokana na shughuli za madini,Ukataji holela wa misitu na shughuli nyingine za kibinadamu kwa taasis mbalimbali kama vile makampuni yanayochimba madini ,taasisi za dini na Idara za serikali.

### Kumbi za mikutano

Wakala una kumbi nzuri za kufanyia semina mbalimbali ambazo zimekuwa kivutio kwa watu wengi kutokana na utulivu na madhari ya eneo la wakala. Bei ya kumbi ni nzuri na inavutia wateja wengi hasa wale wanaofanya shughuli za kiserikali.



*Mojawapo ya kumbi za mikutano*

### Machapisho

Wakala imetoa machapisho mbalimbali ya kitaalamu kuhusiana na masuala ya mbegu za miti. kama ifuatavyo:

- Orodha ya mbegu za miti na bei zake
- Mwongozo wa upandaji na utunzaji wa miti ya mbao, matunda na matumizi mengine Tanzania
- Maelekezo ya jinsi ya kuotesha mbegu za miti
- Kalenda ya ukusanyaji wa mbegu (Seed collection calendar


**ANUANI ZETU**

**MAKAO MAKUU na KANDA YA MASHARIKI NA KATI**
Kihonda, Kilomita 3 kutoka kituo cha mabasi cha Msamvu
Barabara ya Dodoma,
S.L.P 373, Morogoro, Tanzania
Simu: 0626578465 au 0626578472
Email: ttsahq@ttsa.go.tz, eastcentralzone@ttsa.go.tz
Anwani ya mtandao ni www.ttsa.go.tz

**KANDA YA KUSINI MAGHARIBI**
Kibwabwa, Kilomita 3.7 kutoka kituo cha mabasi cha Ipogoro,
Barabara ya kwenda Mbeya,
S.L.P 1121 Iringa
Simu: 0626578502 au 0765891290
Email: southwesternzone@ttsa.go.tz.

**KANDA YA KASKAZINI**
Barabara ya kwenda Magamba karibu na kituo cha utafiti
(Silviculture)
S.L.P. 258, Lushoto
Simu: 0626 578 476
Email: northenzone@ttsa.go.tz

**KANDA YA ZIWA**
Km 5 toka barabara kuu ya Shinyanga – Mwanza,
Barabara ya old /Shinyanga
S.L.P 167 Shinyanga
Simu 0626578518
Email: lakezone@ttsa.go.tz;


**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**

# WAKALA WA MBEGU ZA MITI (TTSA)


TTSA
TANZANIA TREE SEED AGENCY




***Mbegu za miti ni Hazina***

## Utangulizi

Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania (Tanzania Tree Seed Agency – TTSA) ni Wakala wa serikali katika wizara ya Maliasili na Utalii ulioanzishwa mnamo tarehe 24 Januari 2003 kwa mujibu wa sheria ya wakala wa serikali na. 30 ya mwaka 1997 pamoja na marekebisho ya sheria hiyo na 13 ya mwaka 2009. Aidha Wakala wa Mbegu za Miti umeanzishwa kutokana na Mabadiliko ya Program ya Utumishi wa umma (Public Service Reform Program –PSRP) ili kusaidia kuimarisha upatikanaji endelevu wa mazao ya misitu na utunzaji wa mazingira humu nchini kwa kuzalisha, kukusanya na kusambaza mbegu bora za miti pamoja na vipandikizi vingine.




*Jinsi ya kufika makao makuu ya wakala*

## Mahali Ulipo

Makao makuu ya Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania (TTSA) yapo Morogoro mjini,Kilomita tatu kutoka kituo kikuu cha mabasi yaendayo mikoani cha Msamvu, pembezoni mwa barabara iendayo Dodoma. Aidha Wakala unasambaza mbegu bora za miti na Vipandikizi vingine Tanzania kwa kutumia ofisi zake za kanda kama vile Mashariki na kati (Morogoro), Nyanda za juu kusini na Magharibi (Iringa), kanda ya kaskazini (Lushoto) na kanda ya Ziwa (shinyanga).

## Madhumuni

Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania una madhumuni makuu matatu:

- Kuzalisha na kusambaza mbegu bora za miti na vipandikizi vya miti humu nchini kwa matumizi mbalimbali.
- Kutoa ushauri wa kitaalamu ili kuleta uelewa na kuwezesha wateja/wadau kuzalisha miche ya miti kwa mafanikio makubwa kutokana na mbegu zilizozalishwa na kusambazwa na Wakala.
- Kujenga Wakala wenye uwezo endelevu kifedha.

## Dira

Kuwa kituo bora na cha kuigwa katika kuzalisha na kusambaza mbegu bora za miti na vipandikizi vingine katika kanda ya Afrika mashariki na kati.



*Afzelia Quanzensis Seed*

## Dhima

Kuimarisha upatikanaji endelevu wa mazao ya misitu na utunzaji wa mazingira nchini kwa kuzalisha, kukusanya na kusambaza mbegu bora za miti pamoja na vipandikizi vingine.

## Uzalishaji na usambazaji wa mbegu za miti

Wakala unazalisha na kusambaza wastani wa tani 12.5 za mbegu za miti mbalimbali nchini na nje kila mwaka. Wakala pia ina akiba ya tani kati ya 10 mpaka 13 kwa ajili ya kuhudumia wateja wake wakati wowote. Aidha wakala inavyo vyanzo 360 vya miti mbalimbali ikiwepo ya asili na ya kigeni kwa ajili ya kuzalisha mbegu. Wakala inahudumia wateja wastani wa 500 kila mwaka ikihusisha wateja wakubwa kama wakala wa huduma za misitu (TFS,,Idara za serikali, Mashirika ya Umma,Vyama vya ushirika, Makampuni ya watu binafsi,Taasisi za serikali, Taasisi zisizo za kiserikali, Vyuo mbalimbali, taasisi za utafiti na wateja wanaojitokeza mojammoja.

## Aina ya mbegu na miche ya miti inayozalishwa

Wakala una aina Zaidi ya 150 ya mbegu za miti za asili na kigeni zinazozalishwa katika vyanzo mbalimbali nchini. Miti hiyo inamatumizi mbalimbali kama vile mbao, kuni, kivuli, matunda, madawa, kuzuwia mmomonyoko wa udongo.

Aidha wakala unazalisha miche ya miti ya asili na kigeni kwa matumizi mbalimbali. Baadhi ya aina ya miche inayozalishwa na wakala ni pamoja na Mninga, Mkongo, Mpingo, Mvinje, Mtiki, Mvule, Mkangazi, Mwalambe na kadhalika kufanya maandalizi ya kuzikusanya kwani mbegu nyingi hazihifadhiwi kwenye magala kama zilivyo mbegu za mazao ya kilimo.



*Miche ya miembe iliyoboreshwa toka TTSA*

Hii ni kwa sababu mbegu nyingi za miti hufa muda mfupi baada ya kukomaa. Wakala pia unazalisha miche ya matunda aina ya Miembe, Michungwa, Michenza na maparachichi yaliyoboreshwa.

## Jinsi ya kupata mbegu toka Wakala

Wateja wanakaribishwa kununua mbegu na miche ya miti moja kwa moja kwenye kituo kilicho karibu nao. Pia wateja wanaweza kununua kwa kuagizia kwa njia ya barua, simu au barua pepe. Na hata kwa kutumia mtandao.

Kwa maelezo zaidi tembelea mtandao wetu kwa anwani ya www.ttsa.go.tz.Mbegu zitakazoagizwa mapema ndizo zitakazoshughulikiwa kwanza. Hivyo mteja anashauriwa kuagiza mbegu mapema kabla ya msimu wa kupanda. Agiza mbegu zako mapema hata miezi sita kabla ya kuzihitaji ili tuweze kuziandaa mapema.